



Ushauri baada ya kiwewe ya meno

Meno ambayo yamejeruhiwa yanaweza kupata matatizo miezi au hata miaka mingi inayofuata kiwewe. Ni muhimu kuwa meno yaliyojeruhiwa yanakaguliwa mara kwa mara na mtaalamu wa meno.

Wazazi/walezi wanakuwa na wajibu muhimu katika kutunza meno yaliyojeruhiwa. Unaweza kusaidia kwa:

- Kufuata ushauri uliotolewa na mtaalam wa meno
- Kuhakikisha eneo lililojeruhiwa linakuwa safi iwezekanavyo:
 - Kupiga mswaki kwa upole 2 x siku
 - Suuza mdomo na maji joto yenye chumvi baada ya chakula
- Wasiliana na kliniki ya meno ikiwa unaona:
 - badiliko lolote la rangi kwenye jino/meno ambayo imejeruhiwa. (Kielezo cha 1)
 - maumivu yoyote au uvimbe / chunusi unayohusika na jino lililojeruhiwa (Kielezo cha 2)



Kielezo cha 1:
Jino lililozidiwa
kuwa nyeusi



Kielezo cha 2:
Uvimbe kati ya meno
mawili ya mbele

Matibabu ya meno yaliyojeruhiwa yanaweza kuhusisha idadi ya matembezi. Hizi zinaweza kuwa pamoja na:

- Matibabu ya dharura kwa jino lililojeruhiwa na mdomo
- Radiografu za kupima uponyaji
- Kijazi cha rahisi ili kutengeneza "jino lililokatwa"
- Matibabu ya mizizi ya meno kwa majeraha makali zaidi.

Miasi ya ukaguzi inaweza kutakiwa kwa takriban muda wa miezi 3, 6, 12 na 24 ili kuangalia uponyaji na kutathmini kwa matatizo. Katika baadhi ya matukio, mtoto wako anaweza kuelekezwa kwa mtaalamu ili kupata matibabu kwa sababu ya ugumu wa jeraha. Ikiwa mwelekezo unahitajika, wazazi/walezi watakuwa wajibu kwa malipo ya ada.

Tafadhali wasiliana na kliniki kwenye nambari ya simu hapo chini ikiwa unataka maelezo yoyote ziada.



Kwa habari zaidi tafadhali zungumza na mtaalam wako wa meno

Je, unataka habari zaidi au kutoa maoni?

Waraka huu unaweza kupatikana katika miundo mbadala kama vile breli, kanda la sauti au kielektronik kwa ombi.

Afisa wa Mawasiliano, Huduma ya Afya ya Meno
Locked Bag 15, Bentley Delivery Centre, WA 6983

@ publications@dental.health.wa.gov.au

(08) 9313 0555
www.dental.wa.gov.au

Picha zozote zinazotumiwa katika waraka huu ni kwa madhumuni ya kielelezo pekee, kwani zinatolewa tu kama mwongozo wa jumla



© 2020 Dental Health Services WA. All rights reserved.